KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 23, Issue 3

25th Rajab 1433

15th JUNE, 2012

AS-HAAB UL-A'RAAF

NA: ABDUL-HALIM IBN MUHAMMAD NASSAR AS-SALAFI

WATAKAPOKUWA WATU WA "*AL-A'RAAF*" KABLA YA KUINGIA PEPONI

Watu wa "Mahali Paliponyanyuka" wametajwa katika Qur'an kwenye Surah iliyopewa jina lao. *Al-A'raaf*. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na baina yao (hao watu wa Peponi na Motoni) kutakuwa na mahali pa watu wengine (watu ambao bado hawajasamehewa vijidhambi vyao vidogo ili wende Peponi). Na juu ya mahala hapo palipoinuka watakuwako watu hao watakaowafahamu wote (wa Peponi na Motoni) kwa alama zao; na watawaita watu wa Peponi (kuwaambia): 'Assalamu alaykum' (amani iwe juu yenu). Wao (wenye vijidhambi hivyo) bado hawajaingia humo (Peponi) lakini wanatumai. Na macho yao yanapogeuzwa kwenye watu wa Motoni, husema: "Mola wetu! Usituweke pamoja na watu madhalimu (hawa; tusamehe makosa yetu tuingie Peponi). Na hao wa mahali paliponyanyuka watawaita watu (wa Motoni) wanaowafahamu kwa alama zao, waseme: "Haukukusaidieni wingi wenu (huko) wala (vile) mlivyokuwa mkijivunia. (Wazidi kuwasimanga kwa kuwaambia), 'Jee hawa (waliotiwa Peponi) sio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Allaah hatawafikishia rehma? (Mnaona sasa; wameambiwa) 'Ingieni Peponi, hakuna khofu juu yenu, wala hamtahuzunika.'"** Surah al-A'raaf 7:46-49]

Katika aya zilizo hapo juu, Allaah anatupasha habari yakwamba kutakuwepo na kizuizi cha kutenganisha baina ya Pepo na Moto na akafahamisha vyema yakwamba kizuizi hicho kitakuwa ni Ukuta alioutaja katika Surah al-Hadeed katika matamshi Yake: **"Siku watakaposema Wanafiki wanaume na wanafiki wanawake kuwaambia walioamini: 'Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.' Waambiwe (kwa stihizai): 'Rudini nyuma yenu mkatafute nuru yenu. Labda mumeisahau." Utiwe baina yao ukuta wenye mlango; ndani yake mna rehma na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu."** [Surat al-Hadeed 57:13]

Kwahivyo, Pepo itakuwa ndani ya Ukuta na Moto utakuwa nje yake. Na ni ndio ukuta huo ambao Allaah (سبحانه وتعالى) alioukusudia kuwa ndio *"Al-A'raaf*. [Tizama katika *Tadhkirah Al-Arib* cha Ibn al-Jawzi 1/178; *Tafsir al-Manaar* 8/430 na *Adwaa' Al-Bayaan* 2/300]

Ibn Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: "Maana ya *Al-A'raaf* ni mahali palipoinuka juu". Na pia akasema: "Ni mlima ambao unaotumika kama ukuta wenye kuziba baina ya Pepo na Moto. Mlima wenyewe una kishungi (au kilele) kama cha Jogoo. [Tizama katika *Tafsir Mujaahid* 1/237; na *Tafsir At-Tabari* 12/449]

Kwa muangaza wa maelezo haya. *Al-A'raaf* si katika sehemu ya Peponi wala si katika sehemu ya Motoni. Bali ni ukuta uliojitokeza juu ya makaazi yote hayo mawili na mwenye kusimama juu yake atakuwa na uwezo wa kuwaona wakaazi wa Peponi na wakaazi wa Motoni. [Tizama katika Tafsiri ya *At-Tabari* 12/450]

NI KINA NANI HAO *AS-HAAB UL-A'RAAF*?

Baadhi ya wanavyuoni wamesema: "Hao ni watu ambao mema yao na maovu yao yako sawa; wana mambo mema yenye kiasi cha kuwawezesha kuuepuka Moto, lakini na maovu yao ni mengi kiasi cha kutowaruhusu wao kuingia Peponi. Watu hao watabakia hapo kwenye mlima huo (au muinuko huo) mpaka Allaah atakapowatolea uamuzi kama Atakavyo Yeye na awaingize Peponi kwa Rehma zake. Hii ndiyo rai ya al-Hudhaifah Ibn al-Yaman, Ibn Abbaas, Ibn Mas'ud (رضي الله عنهم) - na idadi ya wanavyuoni miongoni mwa watu wema waliokuja baada yao. [Tizama katika *Kitaab az-Zuhd* cha Hanad 1/151; *Tafsir at-Tabari* 12/452; *Tadhkirah al-Arib* 1/179; *Tafsir al-Qur'an al-Adheem* 3/414; na *al-Budur as-Safirah fil-Umur al-Aakhirah* Uk. 279].

Baadhi ya wanavyuoni wamesema yakwamba wao ni watu wema ambao ni wasomi na wanavyuoni; baadhi yao wamesema yakuwa ni Mitume na baadhi nyengine wamesema yakuwa ni *ma-Shuhadaa'*.

Baadhi nyengine wamesema yakuwa ni baadhi ya waumini wazuri waliomaliza kutekeleza katika shughuli zao, kisha wakajitolea wakati wao kuyaangalia matakwa ya wenzao.

Baadhi nyengine wamesema kuwa ni watoto waliozaliwa kutokamana na uzinifu [Tizama katika *al-Budur as-Safirah fil-Umur al-Aakhirah* Uk. 298; na *Fat-hul Qadeer* 2/207].

Juu ya yote hayo, linaloashiriwa na aya ni kwamba wao watakuwa ni watu watakaokuwa miongoni mwa wakaazi wa Peponi ambao kuruhusiwa kwao kuingia Peponi kutacheleweshwa kutokana na sababu zitakazojiri [Tizama katika *Al-Jaami' li Ahkaam al-Qur'an* 4/7/212].

Rai ya idadi kubwa ya wanavyuoni ni kwamba, wao ni watu wenye kiwango kilicho sawa cha mambo mema na maovu; na ambao mema yao hayana uzito unaostahiki wao waingie Peponi,

YALIYOMO

AS-HAAB UL-A'RAAF	1 - 2
SWALA YA MAITI	2 - 3
WAJUE MALAIKA [2]	3 - 4

(Endelea Kutoka Uk. 1)

na kiwango cha maovu yao si kibaya kinachowastahiki wao kuingia Motoni. Kwahivyo, matokeo yake ni kwamba, watasimamishwa juu ya huo muinuko (*al -A'raaf*) kwa muda apendao Allaah.
Hii ni rai iliyo sawa, kutokana na hadeeth iliyopokewa na at-Tabari kutoka kwa 'Amr bin Jareer aliyepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliulizwa kuwahusu watu wa *al-A'raaf*, nae akajibu: "Hao watakuwa ni watu wa mwisho watakaotolewa uamuzi katika waja wa Allaah (Siku Ya Kufufuliwa). Baada ya Allaah atakapomaliza kutoa uamuzi miongoni mwa waja wake, awaambie: "Nyinyi ni watu ambao mema yenu yamewaepusha na Moto, lakini mukawa ni wapungufu wa kuwafanya muingie Peponi. Mimi nitawaacha huru musiingie Motoni; (haya; sasa) ingieni Peponi mutembee mutakavyo!"
Rai hii vilevile imethibitishwa na du'aa' iliyotajwa kwenye aya; kwani inamfaidisha yule atakaekuwa katika hali ya mema yake na maovu yake yatakapokuwa na uzani ulio sawa, na kwahivyo akawachwa asubiri haliyakuwa hajijui mwisho wake. Allaah atawaweka watu wa kwenye muinuko kwenye hali hiyo ili wapate kuwajua wakaazi wa Peponi kwa alama zao. Watawajua kutokana na nyuso zao nzuri zing'arazo, zikiwa na miangaza ya upeo wa furaha. Watawajua wakaazi wa Motoni kwa nyuso zao mbovu zenye kusononeka, zionyeshazo huzuni ndani ya macho yao. Haya ni kulingana na Ibn Abbaas, Mujaahid na al-Hasan al-Basree.

Allaah (سبحانه وتعالى) ameeleza kuhusu alama za wakaazi wa Peponi na alama za wakaazi wa Motoni kwenye idadi ya aya katika Qur'an, nazo ni kama zifuatazo:
"(Katika) siku ambayo nyuso (nyengine) zitakuwa nyeupe, na nyuso (nyengine) zitakuwa nyeusi." [Aal-Imraan 3:106]
"Nyuso (nyengine) siku hiyo zitang'ara (kweli kweli). Zinamtazama Mola wao. Na nyuso (nyengine) siku hiyo zitakunjana. Zitajua yakuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo." [Al-Qiyaamah 75:22-25]
"Siku hiyo nyuso nyengine zitanawiri. Zitacheka, zitachangamka. Na nyuso nyengine Siku hiyo zitakuwa na mavumbi juu yake. Giza Totoro (kubwa) litazifunika." ['Abasa 80:38-41]
Watu wa hapo kwenye muinuko watawatizama wakaazi wa Peponi na wakaazi wa Motoni.watakapowatizama wakaazi wa Peponi, watawaambia, 'Amani iwe juu yenu!' lakini watakapowaangalia watu wa Motoni, na kuwaona jinsi watakavyokuwa wakiumbuka, watamuomba Allaah asiwahusishe miongoni mwa watenda maovu waliojidhulumu nafsi zao na kujitakia ghadhabu za Allaah na mateso ya udhalilifu. Twamuomba Allaah atusalimu salama.
Katika aya Tukufu, Allaah anatupasha habari yakwamba watu wa kwenye muinuko watatamani kuingia Peponi; na Allaah atawatia matamaniwa hayo kwenye nyoyo zao kama matokeo ya fadhila atakazowatunukia juu yao.
Kwenye aya hiyo hiyo, Allaah (سبحانه وتعالى) ametupasha habari yakwamba watu wa kwenye muinuko, watawalingania baadhi ya watu miongoni mwa wakaazi wa Motoni waliokuwa wakiwajua walipokuwa nao ulimwenguni, na ambao waliokuwa ni viongozi, watawala wa mabavu, viongozi madhalimu. Watawaambia: **"Na hao wa mahali paliponyanyuka watawaita watu (wa Motoni) wanaowafahamu kwa alama zao, waseme: 'Haukukusaidieni wingi wenu (huko) wala (vile) mlivyokuwa mkijivunia."** [Al-A'raaf 7:48]
Mali zao walizokuwa wakizirundika na kuzieka kama akiba hapa ulimwenguni na jeuri zao na madharau mbele ya Haki na wana-adamu wenzao hayatowafalia chochote.
Wakati huohuo, makafiri ambao watakaokuwa ndani ya Moto, wataapa yakwamba watu wa kwenye muinuko (Al -A'raaf) watajiunga nao (humo ndani ya Moto). Na hapo ndipo pale Allaah atakapowaambia kwa kuwakaripia: **"Je, hawa (waliotiwa Peponi) sio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Allaah hatawafikishia Rehema?** [Al-A'raaf 7:49]. Matamshi haya ni ya kuwashutumu na kuwalaumu kutokana na kejeli zao walizokuwa wakizitamka dhidi ya Waislamu madhaifu ulimwenguni. Kisha Allaah (سبحانه وتعالى) atawaamrisha watu wa kwenye muinuko (*Al-A'raaf*) waingie Peponi, nao wataingia kwa Rehma Zake zilizoenea juu ya kila kitu. Allaah akasema: **"Sikilizeni! Vipenzi vya Allaah hawatakuwa na khofu (siku ya Kiyama) wala hawatahuzunika. Nao ni wale walioamini na wakawa wanamcha Allaah (wanafuata amri Zake na wanajiepusha na makatazo yake)."** [Yunus 10:62-63]

SWALA YA MAITI

WUDHOO': Jee, anahitajika mtu kuwa na wudhoo' kwa ajili ya swala ya *Janaazah*?
JAWABU: Hakuna taarifa ya waziwazi katika Sunnah kuhusiana na suala hilo. Lakini hatahivyo, sisi tungelipendekeza kwa mkazo kabisa jambo hilo, kwa sababu hukmu ya ujumla ya swala kwa kawaida inahusu pia swala ya Janaazah, na kwa sababu ndani yake muna usomaji wa Qur'an, dhikr na du'aa', ambayo yanahitajika kusomwa na mtu akiwa katika twahara ki-ukamilifu.

KUSWALI KWA JAMAA'AH:
Kama zilivyo swala tano za faradhi, ni waajib kuswaliwa swala ya Janaazah kwa Jamaa'ah. Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya kwa kawaida Mtume (صلى الله عليه وسلم), na akawaamrisha Waislamu wafuate mfano wake kwenye swala aliposema: "Swalini kama mulivyoniona mimi nikiswali."
Lau kama watu wataswali kila mmoja peke yake, uwajibikaji utakuwa umetekelezwa, lakini watakuwa na madhambi ya kuwacha Jamaa'ah - Allaah ndiye Mjuzi zaidi. Imaam an-Nawawee (رحمه الله) amesema: "Hakuna ikhtilafu (miongoni mwa wanavyuoni) yakwamba inaruhusiwa kuswali Janaazah kila mmoja peke yake. Lakini Sunnah ni kuiswali kwa Jamaa'ah, kutokana na hadeeth iliyo swaheeh kuhusiana na suala hili, pakiwa na ziyada ya maafikiano ya wanavyuoni.
Mtu hwenda akashangaa na kujiuliza: "Basi mbona Maswahaba walimswalia Mtume (صلى الله عليه وسلم) kila mmoja kivyake bila ya kuwepo Imaam?" Imaam Ibn Hajar amesema kuhusiana na hayo: "Amesema Ibn Duhyah, 'Ukweli ni kwamba, Waislamu walimswalia kila mmoja peke yake bila ya kuwepo Imaam. Imaam Ash-Shaafi'i akathibitisha yakwamba hii ilikuwa ni kutokana na darajan Kubwa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) - Babangu na Mamangu wawe ni kikombozi chake na kwamba walisisitiza yakwamba pasitokee mtu yoyote atakaeongoza swala ya kumswalia yeye'. Na Allaah yanamuelea zaidi.

(Endelea katika Uk. 3)

(Endelea kutoka Uk. 2)

Hili lilikuwa ni tukio maalum ambalo kwa hakika ni gumu kulieleza na, kwahivyo, hatuwezi kuliachilia mbali kwa ajili ya tukio hilo, jambo ambalo alilolishikilia kulifanya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama kawaida yake alipokuwa akiishi. Hapana shaka yoyote yakwamba uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiwo unaotangulizwa kwa sababu ndio ulio wa sawa na kuthibitishwa kwa njia iliyo bora zaidi.

NI NANI ANAEPASWA KUONGOZA SWALA? **[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO].**

(Endelea kutoka Vol 23, Issue 2)

... kisha mmoja wa Malaika anasema, “Iakini miongoni mwao palikuwa na mmoja wao ambae si katika wao. Yeye alijileta tu kwa ajili ya kitu fulani.” Allaah atasema, “Hata yeye pia nimemsamehe, kwa sababu tu alikuwa amekaa nao. Mtu yoyote atakaekaa na watu hao, basi hatokosa kitu.” [al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه).

MALAIKA HUONA HAYA.

Malaika huwaonea haya watu wema. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alielezea hayo kwa Maswahaba wake vipi Malaika walivyokuwa wakimuonea haya ‘Uthmaan Bin ‘Affaan (رضي الله عنه). Alisema (صلى الله عليه وسلم), “Nisimuonee haya mtu huyu, wakati hata Malaika wamuonea haya?”

HAWAPENDI HARUFU MBAYA

Malaika hawapendezwi na vitu vibaya visivyopendwa na binadamu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Mtu anapokula kitunguu-thaumu, kitunguu-maji, au chakula chochote chenye harufu mbaya, na asiikurubie misikiti yetu, kwa hakika Malaika huchukizwa na vitu vilevile vyenye kumchukiza Mwana wa Adamu. [Muslim].

HAWAPENDI MAJIBWA AU MAPICHA

Malaika hawaingii kwenye nyumba zenye mbwa au picha za wana-adamu au wanyama, kwa sababu Allaah ameviharamisha vitu hivyo. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Kwa hakika Malaika hawaingii kwenye nyumba yenye mbwa au picha [al-Bukhari na Muslim].

ADABU ZA MALAIKA MBELE YA ALLAAH

Malaika ni miongoni mwa viumbe vya Allaah walio bora. Kwa ajili hii, amewachagua wao kwa kazi zilizo muhimu, na akawaruhusu wengi wao wawe karibu Naye. Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema: **“Masihi (’Issa mwana wa Maryam) hataona unyonge kuwa mja wa Allaah, wala Malaika waliokurubishwa (na Allaah hawataona nyonge kuwa waja wa Allaah).”** [an-Nisaa’ 4:172].

MALAIKA WANAMUABUDU ALLAAH DAIMA-DAWAMA

Malaika wanamuabudu Allaah kwa njia nyingi tafauti, pasi na kusita. Wao huswali kwa ajili Yake, hufanya Tasbeeh, hufanya Hajj, na kadhaalika. Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema: **“Wanamtukuza Usiku na Mchana, hawanyong’onyei (hawafanyi uvivu).”** [al-Anbiyaa’ 21:20]. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Njia bora za kumkumbuka Allaah ni ile aliyowachagulia Malaika Wake. **SUBHAANALLAAH WA BI-HAMDIH.**” [Muslim, Abu Dharr].

MALAIKA HUSWALI WAKIWA KWENYE MISTARI ILIYO NYOOKA.

Malaika huswali mbele ya Allaah wakiwa kwenye mistari iliyo nyooka sawasawa. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **“Naapa kwa (wale Malaika) wajipangao safusafu. Tena kwa wale wanaokataza mabaya. Kisha kwa wale wasomao mawaidha (ya Allaah).”** [as-Swaafaat 37: 1-3]

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Nyinyi hamupendi kupanga swafu zenu kama Malaika wanavyojipanga mbele ya Mola wao? Wao hukamilisha swafu ya kwanza kisha wakaunga nyengine na nyengine...”

MALAIKA HUSUJUDU

Malaika huswali mbele ya Mola wao kwa kusimama, kwa ku-rukoo’, na kusujudu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Mbingu zimetingishika (kutokana na uzito), na zina haki ya kutingishika: kila sehemu ndani yake yenye nafasi kiasi cha msamba mmoja wa mkono imechukuliwa na Malaika akiwa anasujudu au amesimama (kwa ajili ya kuswali).

MALAIKA HUWENDA HAJJ

Tumejifunza pia kuhusu idadi kubwa ya Malaika kutokana na aliyotueleza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu al-Bayt ul-Ma’moor. Hii ni nyumba iliyoko kwenye Wingu ya saba, mfano wa Ka’bah katika ardhi hii. Malaika wanaitembelea nyumba hiyo kwa ajili ya kumuabudu Allaah (سبحانه وتعالى). Miongoni mwa wale wanaoingia humo kila siku,Elfu-Sabiini hawatoki tena humo mpaka siku ya kuhukumiwa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Kwa hakika, Malaika wapya Elfu-Sabiini wanaingia ndani ya Bayt Ul-Ma’moor kila siku, na hawatoki tena kutoka humo.”

MALAIKA HUMCHA ALLAAH

Malaika wanamjua Allaah vilivyo ndio ikawa wanamcha ipasavyo. Allaah (سبحانه وتعالى) ametueleza jinsi Malaika wanavyomcha Yeye: **“Na vinamsujudia Allaah vyote venye uhai mbinguni na katika ardhi katika wanyama na Malaika pia nao hawatakabari. Wanamuogopa Mola wao aliye juu yao na wanatenda wanayoamrishwa.”** [AN-NAHL 16:49-50]**.**

Hata Jibreel anamuogopa Allaah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Katika Usiku wa Israa’, nilipita karibu na Malaika walio juu zaidi, Jibreel alionekana kama zulia lililofumuka (lililochakaa) kutokana na khofu ya Allaah.

MALAIKA WANAMTWI’ ALLAAH

Malaika ni watwiifu mno kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na wala hawamu’asi kwa lolote. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى) kuwahusu wao: **“Na makafiri wanasema: ‘(Allaah) Mwingi wa Rehema amejifanyia mtoto.’ Ametakasika (Allaah!) Bali (hao Malaika) ni waja (wa Allaah) waliotukuzwa. Hawamtangulii kwa neno (lake analosema). Nao wanafanya amri Zake (zote).”** [al-Anbiyaa’ 21: 26-27]

MALAIKA WANAPENDA APENDACHO ALLAAH

Malaika wanapenda apendacho Allaah au anachowaamrisha Allaah wakipende. Kwahivyo, wao humpenda mtu anaependwa na Allaah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Allaah anapompenda mtu (mzuri), humlingania Jibreel (عليه السلام) na kumwambia, ‘Mimi nampenda mtu huyu, kwahiyo na wewe mpende.’ Jibreel nae akampenda mtu huyo. Kisha Jibreel nae akaanza kulingania Mbinguni, ‘Allaah anampenda mtu huyu, kwahiyo nanyi mpendeni.’ Basi Malaika wote wa Mbinguni nao wakampenda mtu huyo.” [al-Bukhaari, Muslim, na wengineo kutoka kwa Abu Hurairah].

Kama tulivyotaja hapo awali, Malaika pia hupendezwa na mikusanyiko yenye kumpendeza Allaah. Kwahiyo, wao (Malaika) hupenda kuketi miongoni mwa wenye kuswali, kusoma Qur’an, wenye kumtaja Allaah, au

wenye kusema jambo lolote lililo zuri. Makafiri wanasema yakwamba kuna Malaika wa mapenzi aitwae “Cupid”. Wamempa taswira (picha) ya kijana barobaro aliyebeba Uta na Mkuki. Anapotupa mshale wake baina ya watu wawili, hapohapo wataanza kupendana. Haya yote si maneno ya kweli, na hatufai sisi kuyaamini maneno hayo.

MALAIKA HUSHUKA KWA AMRI YA ALLAAH

Malaika hawashuki kutoka Mbinguni kila wapendapo wao wenyewe. Wao hushuka kwenye ardhi hii pale wanapoamrishwa kushuka na Allaah (سبحانه وتعالى) peke yake. Ibn ‘Abbaas (رضي الله عنه) amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia Jibreel (عليه السلام): “Kwanini wewe huji kwetu kila zaidi ya unavyokuja?” Mara Allaah (سبحانه وتعالى) akateremsha katika Qur’an: **“Sisi (Malaika) huwa hatushuki isipokuwa ni kwa amri ya Mola wako. Kila kilichoko mbele yetu na nyuma yetu ni vyake Yeye.”** [Surat Maryam 19:64. (al-Bukhaari)]

MALAIKA WAKIWA PAMOJA NA WAUMINI

Malaika ni marafiki wa Waumini. Hufanya kila juhudi ili wawasaidie na kuwalinda

MALAIKA HUWAOMBEA WAUMINI DU’AA’

Malaika humlingania Mola wao na kumuomba awasamehe waumini, awalinde na adhabu, na awaingize Peponi. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **“Wale wanaokichukuwa Kiti cha Enzi (cha Allaah) na wale wanaokizunguka, wanamtukuza Mola wao na kumsifu na wanamuamini na wanawaombea samahani walioamini, (wanasema): ‘Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa Rehma na ilimu (Unakijua kila kitu). Basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako na waepushe na adhabu ya Jahanamu. Mola wetu! Waingize katika Mabustani ya milele uliyowaahidi. Na uwape haya pia waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao; bila shaka Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima. Na waepushe na maovu, kwani umuepushaye na maovu siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa.”** [Ghaafir 40:7-9]

MALAIKA HUITIKIA ’AAMEEN WANAPOSIKIA DU’AA’

Pindi Muislamu anapomuombea Du’aa’ Muislamu mwenzake, kuna Malaika huitikia kwa kusema ’Aameen. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Du’aa’ ya Muislamu kwa mwenzake awapo hayuko, hutakabaliwa (na Allaah). Huwa kuna Malaika anaebaki hapo kando ya kichwani chake, na kila anapomuombea Muislamu mwenzake kitu kizuri, yule Malaika husema, “Aameen! Nawe ulipwe kama hilo ulomuombea.” [Muslim, kutoka kwa Abud-Dardaa’].

Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Kwa hakika, pindi Imaam (awapo kwenye swala) anaposema “Aameen!” Malaika nao pia husema “Aameen.” kwahivyo yoyote atakaesema “Aameen” wakati mmoja na Malaika, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia.” [Bukhaari na Muslim]

MALAIKA WANAWASHUFAIYA WAUMINI

Kwa kutokana na ruhusa ya Allaah, Malaika wanaweza kuwaombea waumini. Kuwaombea kwa maana ya “Kumuomba Allaah awasamehe na kuwaokoa na adhabu. Kwahivyo ni sampuli ya du’aa’ au maombi. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: “**Na wako Malaika wangapi Mbinguni, ambao uombezi wao hautofaa chochote isipokuwa baada ya Allaah kutoa idhini kwa Amtakaye na kumridhia.”** [an-Najm 53:26]

MALAIKA HUKAA NA WAUMINI

Malaika daima huwa pamoja na waumini - isipokuwa wakati wanapovua nguo zao au wanapoingia Chooni. Wao huwalinda na maangamivu na vitendo vibaya. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Kuna makundi mawili ya Malaika wanaokaa na nyinyi katika wakati wa usiku na wakati wa mchana. Wote hao hukutana wakati wa swala za *al-Fajr* na *al-Asr*. Wale waliopitisha wakati pamoja na nyinyi usiku, hurudi juu Mbinguni, na Allaah huwauliza, ingawaje anayajua yote yaliyowatokea nyinyi, “Mumewaachaje waja wangu?” Malaika hujibu, “Tulipowaacha, walikuwa wakiswali; na pia tulipowarudia, tuliwakuta wakiswali.” [al-Bukhaari kuitoka kwa Abu Hurairah]

MALAIKA HUWASAIDIA NA KUWALINDA WAUMINI

Malaika wanawapenda waumini na wanawalinda kutokamana na ma-Jinni, ma-Sheitwani, maafa na madhara. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **Ana (kila mtu) kundi (la Malaika) mbele yake na nyuma yake; wanamlinda (na kuyadhibiti anayoyafanya) kwa amri ya Allaah.”** [Ar-Raa’d 13:11. Sasa ni kwanini Malaika wanawalinda waumini? Na ni kwanini wanakaa nao kila mahali? Jawabu ni kwamba, mu’min kila wakati huwa anajaribu kumtwi’i Allaah na Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) na kutenda mambo ya kheri. Anajaribu kudumu kumkumbuka Allaah (سبحانه وتعالى) - kwa ulimi wake na moyo wake. Kuna njia nyingi ambazo mu’min huwa katika kumtaja Mola wake. Hatuwezi kuanza kuzitaja njia hizo kutokana na wingi wake.. Hii ndiyo sababu Malaika humlinda mu’min na kumpenda.

MALAIKA HUPIGANA WAKIWA UPANDE WA WAUMINI

Malaika walipigana katika vita vingi wakiwa katika upande wa Waislamu. Kwa mfano, Allaah (سبحانه وتعالى) amesema kuhusu vita vya Badr: **“(Kumbukeni) Mola wako alipowafunulia Malaika (akawaambia): ‘Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu wale walioamini; nitatia uoga katika nyoyo za makafiri. Basi wapigeni juu ya shingo (zao) na kateni kila ncha za vidole vyao.”** [al-Anfaal 8:12]

Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema siku hiyo: “Mimi nilimuona Jibreel amekizuiya kichwa cha Farasi wake akiwa tayari kwa vita na silaha zake.”

MALAIKA HUWAAMBIA WAUMINI WAWE WATU WEMA

Mashetwani huwanong’oneza watu wafanye mambo mabaya. Lakini Malaika huwanong’oneza waumini wafanye mambo mazuri. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “kila mmoja wenu ana mwenzake miongoni mwa ma-Jini na Malaika.” Maswahaba waliposikiya maneno hayo, wakamuuliza, “Hata wewe, Ewe Mtume wa Allaah?” Akawajibu, “Ndio, hata mimi pia. Lakini Allaah amenisaidia kumfanya awe ni Muislamu. Kwahivyo, yeye huniamrisha mimi kutenda mema tu.” [Muslim, kutoka kwa Ibn Mas’ud]. Kuna Malaika wanaowalingania watu watoe pesa kwa njia ya Allaah. Maana yake ni kutoa pesa kuwasaidia masikini, kujenga misikiti, kufundisha watu Uislamu na Qur’an, na kadhaalika... Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: “Katika mapambazuko ya kila siku, Malaika wawili hushuka (kutoka Mbinguni). Mmojawapo husema, ’Yaa Allaah, mzidishie pesa mtu yoyote atakaetumia (katika njia yako).’ Na yule mwengine nae husema, “Yaa Allaah, zitokomeze pesa za mtu yoyote asiyetaka kutumia (katika njia yako).’” [al-Bukhaari, kutoka kwa Abu Hurairah]. Ndiyo kama ilivyo, sisi huwa hatuwasikii hao Malaika, lakini tunahisi wanayoyasema, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametwambia kuyahusu hayo.